**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KURUGENZI YA MAWASILIANO YA RAIS, IKULU**

*Dodoma*
*13 Januari, 2026*

Baruapepe: press@ikulu.go.tz

# TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

## RAIS SAMIA AFUNGUA MKUTANO MKUU WA MWAKA WA CHAMA CHA MAHAKIMU NA MAJAJI TANZANIA (TMJA)

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, amefungua rasmi Mkutano Mkuu wa Mwaka wa Chama cha Mahakimu na Majaji Tanzania (TMJA) mkoani Dodoma.

Rais Dkt. Samia alisema Mahakama ni taasisi ya msingi katika ujenzi wa Taifa linalozingatia utawala wa sheria, haki, na maendeleo endelevu, na kusisitiza kuwa hakuna mfumo mbadala unaoweza kuchukua nafasi ya Mahakama huru na inayoaminika.

Aidha, alibainisha uhuru wa Mahakama kuwa sharti la msingi la upatikanaji wa haki kwa wananchi na ni msingi wa imani ya umma kwa taasisi za dola, sambamba na kutoa rai ya uwajibikaji, uadilifu, nidhamu na kuzingatia viapo vya kazi vya Mahakimu na Majaji.

Katika hilo, alisisitiza dhamira ya Serikali ya kuendelea kujenga Taasisi ya Mahakama yenye hadhi ya kimataifa, akibainisha kuwa Mahakama huru na yenye ufanisi ni msingi wa utawala wa sheria, haki na maendeleo ya Taifa.

Alisema Serikali itaendelea kuheshimu mipaka ya kikatiba ya Mahakama huku ikiimarisha mazingira ya kazi yatakayowezesha utoaji haki kwa ufanisi, uwazi na kwa wakati unaokidhi matarajio ya wananchi.

Katika hatua nyingine, Rais Dkt. Samia alifafanua mageuzi ya kimkakati yaliyotekelezwa na Serikali ya Awamu ya Sita katika sekta ya haki, yakiwemo maboresho ya miundombinu ya Mahakama, ongezeko la rasilimali watu, uboreshaji wa maslahi ya watumishi, pamoja na matumizi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano katika uendeshaji wa mashauri na shughuli za kiutawala za Mahakama.

Aliongeza kuwa, hatua hizo zinalenga kukuza ufanisi wa Mahakama, kupunguza ucheleweshaji wa mashauri, na kuimarisha uwajibikaji na uwazi katika utoaji wa haki kwa wakati kwa wananchi.

Vilevile, alidokeza nafasi ya kimkakati ya Mahakama katika utekelezaji wa Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050, hasa katika kulinda utawala wa sheria, kudumisha amani, na kuhakikisha utulivu wa kisiasa na kijamii.

Halikadhalika, aliwataka Majaji na Mahakimu kuendelea kutekeleza majukumu yao kwa weledi na ujasiri, akisisitiza kuwa imani ya wananchi kwa Mahakama ni rasilimali ya Taifa inayopaswa kulindwa na kuimarishwa kupitia vitendo na maamuzi ya haki.

Kwa upande wake, Jaji Mkuu wa Tanzania, Mheshimiwa George Mcheche Masaju, alisema mageuzi yanayofanywa na Serikali katika sekta ya haki yanalenga kuiweka Mahakama ya Tanzania katika viwango vya kimataifa vya ubora wa mifumo ya haki duniani.

Jaji Mkuu Masaju aliainisha vigezo tisa vinavyotumika kupima ubora wa Mahakama duniani na kuiomba Serikali kuimarisha maeneo mawili muhimu ambayo ni rasilimali fedha na maslahi ya watumishi wa Mahakama.

Rais Dkt. Samia alikubali maombi hayo na kueleza kuwa yatafanyiwa kazi kwa kadiri uchumi utakavyoruhusu.

Shaaban Kissu
Naibu Mkurugenzi wa Mawasiliano ya Rais, Ikulu